**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA MAMLAKA ZA MIJI**

**SURA YA 288**

**SHERIA NDOGO**

**(Zimetungwa chini ya kifungu 89)**

**SHERIA NDOGO ZA (MAHUDHURIO YA LAZIMA KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI ZA SERIKALI) ZA HALMASHAURI YA MJI WA NZEGA ZA MWAKA 2016**

| | | |
|---|---|---|
| Jina na mwanzo wa kuanza kutumika | 1. | Sheria ndogo hizi ziitwe Sheria ndogo za (Mahudhurio ya Lazima katika Shule za Msingi na Sekondari) za Halmashauri ya Mji wa Nzega za mwaka 2016 na zitaanza kutumika tarehe zitakapotangazwa katika Gazeti la Serikali. |
| Eneo la kutumiwa | 2. | Sheria ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Mji wa Nzega. |
| Tafsiri: | 3. | **Katika Sheria hizi:-**<br>**"Halmashauri**" maana yake ni Halmashauri ya Mji wa Nzega. |
| | | "**Mamlaka inayohusika**" maana yake ni Halmashauri ya Mji wa Nzega, Serikali ya Kijiji au Kamati ya Maendeleo ya Kata. |
| | | **Mwanafunzi"** maana yake ni mtoto aliyeandikishwa shule na inajumuisha mtoto yeyote ambaye hajamaliza Elimu ya Msingi na Sekondari kidato cha nne au sita. |
| | | "**Mzazi"** maana yake ni Baba au Mama wa mtoto aliyeandikishwa shule na inajumuisha mlezi yeyote mwenye dhamana ya kumtunza na kumlea mtoto huyo. |
| | | "**Serikali ya Kijiji**" maana yake ni Halmashauri ya Kijiji ambayo ndiye mmiliki wa shule hiyo ya Msingi. |
| | | '**Shule"** maana yake ni eneo ambapo mtoto anaenda kujifunzia na inajumuisha shule zote za Msingi na Sekondari, za Serikali zilizomo katika eneo la Mamlaka ya Halmashauri ya Mji wa Nzega. |
| | | "**Mtoro**" maana yake ni mwanafunzi ambaye hajahudhuria shule kwa |

| | | |
|---|---|---|
| | | jumla ya siku thelathini au zaidi katika mwaka wa masomo. |
| | | "**Afisa Elimu**" ni mtumishi wa umma mwenye dhamana ya kusimamia elimu ya msingi au sekondari pia anaweza kuwa mtumishi yeyote aliyekasimishwa kutekeleza majukumu ya Afisa Elimu wa Mji wa Nzega. |
| | | "**Mkaguzi wa shule**" ni mtumishi wa umma mwenye dhamana ya kukagua shule za msingi au Sekondari. |
| Kuandikishwa na mahudhurio: Sheria ya elimu) sura 353 kifungu 35(3) | 4. | 1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kila mzazi au Mlezi atahakikisha mtoto wake mwenye umri wa miaka saba (7) anaandikishwa shule kwa ajili ya Elimu ya Msingi au Mwanafunzi aliyechaguliwa kwenda Sekondari anaandikishwa shule na kuhudhuria masomo ya shule hizo mpaka atakapomaliza masomo ya elimu ya msingi au sekondari. |
| | | 2) Mwalimu mkuu au Mkuu wa shule atatakiwa kutoa taarifa ya kila mwezi<br>ya mwanafunzi aliyechaguliwa kwenda Sekondari na aliyendikishwa shule na kuhudhuria masomo ya shule hizo mpaka atakapomaliza masomo ya<br>elimu ya msingi au sekondari. |
| Ukaguzi wa Elimu: sura 353 kifungu cha 41 | 5. | (1)Afisa Elimu wa Mji wa Nzega au Mkaguzi wa shule anaweza kwenda kwenye shule yeyote na kufanya ukaguzi.<br><br>(2)Afisa Elimu wa Mji au Mkaguzi wa shule atawasilisha taarifa ya ukaguzi kwa mamlaka inayohusika ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi ya watu wote watakaovunja Sheria Ndogo hizi. |
| Sheria ya elimu sura 353 kifungu cha 35 (3) | | (3)Mwanafunzi atakayekosa kuhudhuria masomo kwa siku thelathini (30) mfululizo, bila sababu ya msingi atakuwa amehesabiwa kuwa mtoro. |
| Kazi na majukumu ya Kamati au Bodi ya shule: | 6. | Majukumu ya Kamati au Bodi ya shule yatakuwa kama ifuatavyo:-<br>(1)Kuhakikisha kuwa wanafunzi wote walioandikishwa shule wanahudhuria shule hiyo hadi watakapomaliza elimu ya au Sekondari.<br><br>(2)Kuhakikisha kuwa walimu wote waliopo katika shule ya Msingi au Sekondari wanafundisha masomo yote kwa mujibu wa ratiba. |

| | | |
|---|---|---|
| | | (3)Kuhakikisha kuwa watoto hawafanyishwi kazi za nje muda wa masomo.<br><br>(4)Kuhakikisha kuwa wanatoa taarifa kwa maandishi ya wanafunzi watoto kwa Mamlaka inayohusika ili kuchukua hatua zinazostahili. |
| Makosa kwa upande wa Mzazi au Mlezi. | 7 | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi itakuwa ni kosa kwa Mzazi au Mlezi yeyote kwa:-<br><br>(1) Kushindwa kumwandikisha mtoto kuanza Elimu ya Msingi au kushindwa kumpeleka kidato cha kwanza mwanafunzi aliyechaguliwa kujiunga na elimu ya Sekondari.<br>(2) Kumkataza au kumzuia mtoto kuendelea na Elimu ya Msingi au Sekondari au kufanya jambo lolote litakalomfanya mwanafunzi ashindwe kuendelea na masomo.<br>(3)Kumtuma Mwanafunzi kazi yeyote wakati wa masomo.<br>(4)Kumuoza au kusababisha kuolewa.<br>(5)Kutompatia vifaa vya shule na mahitaji mengine muhimu katika kujifunza.<br>(6)Kutofanya jitihada za kumwendeleza mtoto asiyechaguliwa kujiungana masomo ya Sekondari katika shule za Serikali.<br>(7)Kutotoa taarifa juu ya kubadilika kwa tabia ya mwanafunzi. |
| Makosa kwa Walimu | 8. | Itakuwa kosa kwa Waalimu:-<br><br>(1)Kumsimamisha kuhudhuria shule mwanafunzi yeyote kwa kosa ambalo kimsingi halikusababishwa naye bali mzazi wake au mtu yeyote.<br><br>(2)Kumtumikisha Mwanafunzi kazi yeyote ambayo haiko katika mpango wa kazi za shule ambayo haijaidhinishwa na Kamati au bodi ya shule.<br><br>(3)Kutoa adhabu zilizokatwa chini ya Sheria yoyote andishi, na Kanuni au Amri yote chini ya mamlaka yoyote husika.<br><br>(4)Kukataa kwa makusudi mwalimu au kushindwa, kukamilisha kipindi au vipindi alivyopangiwa kufundisha kwa siku hiyo au siku hizo.<br>(5)Kutotoa taarifa ya kipindi cha mwezi mmoja kuhusiana na mimba |

| | | |
|---|---|---|
| | | za wanafunzi.<br><br>(6)Kuanzisha michango isiyo halali itakayowafanya wanafunzi wengi kushindwa kulipa na hivyo kuwa watoro. |
| Makosa kwa Jamii | 9. | Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa sheria hizi kwa mtu yeyote:-<br>(1)Kumwajiri mtoto anayekwenda shule kwa kazi yoyote ile.<br>(2)Kumtorosha kabla ya kumaliza Elimu ya Msingi na Sekondari. |
| Sheria ya makosa ya kujamiiana sura ya 101 ya 1998 kifungu cha 6 | | (3) Kufanya mapenzi na mwanafunzi wa shule au hata kumwandikia Barua za mapenzi au kumshawishi kuacha au kumtorosha masomo au kupiga picha naye za uchi. |
| | | (4) Kumchumbia au kumuoa mtoto wa shule. |
| Makosa kwa Mwanafunzi Sura 13 | 10. | Itakuwa ni kosa kwa mtoto wa shule:-<br>(1)Kutohudhuria shule.<br>(2)Kutoroka vipindi darasani,<br>(3)Kuvunja taratibu za shule husika.<br>(4)Kujiingiza kwenye masuala ya ngono au biashara ya ngono,<br>(5)Kunywa au kuingia kwenye maeneo ya vileo.<br>(6)Kutumia madawa ya kulevya. |
| Adhabu | 11. | (1) Mtu yeyote atakayevunja au kushindwa kutekeleza masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atahukumiwa kulipa faini isiyozidi shilingi mia tatu elfu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au vyote kwa pamoja faini na kifungo. |
| Sheria ya makosa ya kujamiina sura ya 101 kifungu cha 6 | | (2) Mtu yeyote atakayekuwa na mahusiano ya kimapenzi na mwanafunzi atakuwa ametenda kosa, adhabu kali itatolewa kwa mujibu wa sheria ya makosa ya kujamiana sura 101 ambayo kifungo chake ni miaka thelathini. |
| | | (3) Mwanafunzi akipatikana na hatia ataadhibiwa kwa mujibu wa taratibu zinazo simamiwa na kamati ya nidhamu za shule husika kwa kuzingatia Sheria ya Elimu Sura 353 na Sheria ya Watoto na Vijana Sura 13. |

Nembo ya Halmashauri ya Mji wa Nzega imebandikwa kwenye Sheria Ndogo kufuatia Azimio lilipoitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika Tarehe …………………mwaka 2016

…………………………………………..

**PHILEMON M. MAGESA**

**MKURUGENZI MJI NZEGA**

**…………………………………………**

**WILLIAM W.JOMANGA**

**MWENYEKITI HALMASHAURI**

**MJI NZEGA**

**Nakubali………………………………………….**

**Tarehe……………………………………………**

**……………………………..**

**JOHN POMBE MAGUFULI**

**RAIS**

**DODOMA**